**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUCHUNGUZA NA KUDHIBITI HESABU ZA SERIIKALI (PAC) KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU HESABU KWA MWAKA 2020/2021

**Mheshimiwa Spika,** awali ya yote naomba kumshukuru Mwenyenzi Mungu kwa kuendelea kuturuzuku uhai na afya njema na kuweza kufika hapa kwa lengo la kutekeleza majukumu tuliyokabidhiwa na wananchi wa nchi hii.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kukushukuru wewe binafsi kwa niaba ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika ya Baraza la Wawakilishi (PAC) kwa kuniruhusu kuwasilisha maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kumshukuru pia Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Katibu Mkuu, pamoja na Watendaji wote wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mashirikiano makubwa waliyotupatia wakati wa kuchambua na kupitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii.

**Mheshimiwa Spika,** kwa heshima ya upekee napenda kuwashukuru Wajumbe na Makatibu wa Kamati ya PAC kwa moyo wao wa kujituma na umakini waliouonesha na hatimae Kamati hii ikaweza kuipitia, kuichambua na kutoa mapendekezo yake.

**Mheshimiwa Spika,** kwa umuhimu huo, naomba sasa kuwatambua Wajumbe na Makatibu wa Kamati ya PAC kwa kuwataja kama ifuatavyo:

1. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Mwenyekiti.
2. Mhe. Shaib Said Ali - Makamo Mwenyekiti.
3. Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Mjumbe
4. Mhe. Bihindi Hamad Khamis - Mjumbe
5. Mhe. Hamad Abdalla Rashid - Mjumbe
6. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Mjumbe
7. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Mjumbe
8. Ndg. Nasra Awadh Salmin - Katibu
9. Ndg. Haji Khatib Haji - Katibu

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla Kamati ya PAC imeridhika na utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka 2019/2020 pamoja na mapendekezo ya Makidirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii kwa mwaka 2020/2021 kama yalivyoainishwa katika Fungu E 04 la Ofisi hii.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na hayo, Kamati imeona ipo haja ya kuyatilia mkazo baadhi ya mambo machache na muhimu kwa ajili ya utekelezaji bora wa Bajeti hii na kuimarisha utendaji katika Ofisi hii pamoja na kuongeza ufanisi katika Serikali hasa ikizingatiwa kuwa Ofisi hii ni chombo muhimu sana katika kupima na kuimarisha Uwajibikaji na Utawala Bora katika Serikali na katika nchi kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** katika Mapato, inafahamika kuwa ukusanyaji wa mapato katika Ofisi hii unatokana na mapato yanayotokana na ada za ukaguzi wa Mashirika na Taasisi za Serikali pamoja na miradi mbali mbali ya maendeleo inayofadhiliwa na Washirika wa Maendeleo ambapo ada hizo hulipwa baada ya kukamilika kwa ukaguzi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Ofisi hii ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 158,000,000 ambapo hadi kufikia mwezi Machi 2020 jumla ya shilingi 88,930,726 zilikusanywa, sawa na aslimia 56.28 ya makadirio.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa hali hiyo imesababishwa pamoja na mambo mengine na kusuasua na kuchelewa kwa baadhi ya Mashirika na Taasisi za Serikali katika kulipa ada hizo za ukaguzi kunakotokana na uwezo mdogo wa kifedha wa Mashirika na Taasisi hizo likiwemo Shirika la Magazeti na Chuo cha Uandishi wa Habari.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mnasaba huo, Kamati ya PAC inaiomba Serikali kujipanga vizuri zaidi na kuhakikisha kuwa Mashirika na Taasisi hizo zinakuwa na uwezo wa kukidhi za matumizi yao hasa yale yaliyo muhimu yakiwemo ya kulipa ada ya ukaguzi kwa wakati kama taratibu za ukaguzi zinavyoelekeza.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa utekelezaji wa malengo yake mbalimbali kupitia matumzi ya Ofisi hii kwa mwaka 2019/2020, Kamati imefarajika sana kuona kuwa kati ya Wakaguzi 156 waliopangiwa kupatiwa mafunzo, Ofisi hii hadi mwezi Machi 2020 imeweza kuwapatia Wakaguzi wake 136 mafunzo ya ukaguzi yakinifu, ukaguzi wa kiuchunguzi (Forensic Audit) pamoja mafunzo ya viwango vya ukaguzi vya Kitaifa na Kimataifa ikiwa ni sawa na asilimia 87. Aidha, pamoja na kuwepo kwa wafanyakazi 15 wanaoendelea na mafunzo ya muda mrefu katika vyuo mbali mbali, ni faraja pia kuona kuwa kati ya wafanyakazi 31 waliopangiwa kupatiwa mafunzo ya muda mfupi katika kada mbalimbali, jumla ya wafanyakazi 21 wameweza kupatiwa mafunzo hayo ikiwa ni sawa na asilimia 68.

**Mheshimiwa Spika**, kimsingi, hii ni hatua muhimu na ya kupongezwa hasa ikizingatiwa kuwa kazi za Ukaguzi ni kazi ngumu na nyeti ambazo sio tu zinahitaji watendaji wenye moyo wa kujituma, uvumilivu, uadilifu, na umakini lakini pia huhitaji watendaji wenye weledi na ujuzi mkubwa kwenye nyanja zote za ukaguzi na wanaoweza kukabiliana na kasi ya mabadiliko ya teknolojia ya mifumo ya utendaji kazi inayoendelea kukua siku hadi siku.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande mwengine, Kamati inaendelea kuikumbusha na kuisisitiza Serikali juu ya utekelezwaji wa lile suala linalosubiriwa kwa muda mrefu la kuwasilishwa hapa Barazani Ripoti ya Ukaguzi ya Ofisi yenyewe ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kama ambavyo kifungu cha 122(4) na (5) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016 kinavyoelekeza.

**Mheshimiwa Spika,** kama ilivyoelezwa, kwa mwaka 2020/2021 Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inaendelea kutekeleza Programu Kuu mblli ambazo ni Programu ya Udhibiti na Ukaguzi wa Fedha na Rasilimali za Umma na Programu ya Utawala na Uendeshaji wa Udhibiti na Ukaguzi ambapo Ofisi hii imekadiriwa kutumia jumla ya shilingi 4,243,300,000 kwa ajili ya kutekeleza malengo yake katika Programu hizo. Aidha, Ofisi hii inakadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 225,000,000 kutoka katika vyanzo vyake vya mapato.

**Mheshimiwa Spika,** naomba niendelee kukiri kuwa Kamati ya PAC imeyaridhia na kuyaunga mkono mapendekezo hayo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Hivyo basi, nawaomba na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili wayapitie, wayajadili na hatimae wayapitishe Makadirio hayo ili Ofisi hii iweze kutekeleza vyema majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, naomba nimalizie hotuba yangu hii kwa kuwashukuru Wajumbe wa Baraza lako Tukufu, kwa utulivu na umakini wao wa kunisikiliza wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha hotuba hii.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha.

Ahsante,

………………………..
**(Shaib Said Ali)**
**Kny. Mwenyekiti,**
**Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Seriikali (PAC)**
**Baraza la Wawakilishi,**
**Zanzibar**